# Advanced Swahili Syllabus

**UNIVERSITY OF CALIFORNIA BERKELEY**
Department of African American Studies
FALL SEMESTER 2013

| | |
|---|---|
| **Kozi** | **AFRICAN AMERICAN STUDIES 15A P 001 REC** |
| **Mwalimu** | **David Kyeu** |
| **Anwanipepe** | **kyeu@berkeley.edu** |
| **Ofisi** | **654 jumba la Barrows** |
| **Wapi** | **65 EVANS** |
| **Lini** | **Jumanne, Jumatano na Alhamisi** |
| **Muda** | **Saa nne asubuhi hadi saa sita mchana (J4 na J5)**<br>**Saa tano mchana hadi saa sita (Alhamisi)** |
| **Krediti** | **5** |
| **Saa za ofisi:** | **J3: saa kumi na nusu hadi saa kumi na moja na nusu jioni – B-37 Dwinelle**<br>**J5: Saa sita na nusu hadi saa saba na nusu – 654 Barrows** |

**K A R I B U N I**




This tentative syllabus is subject to change depending on your individual, research or academic interests. It is a contract upon which your grade depends. Please read it carefully.

## MAELEZO YA KOZI

**KARIBUNI!** The design of this syllabus is based on standards for teaching Swahili as a foreign language in the United States. To familiarize yourself with the standards, go to the following link: http://www.actfl.org/publications/all/national-standards-foreign-language-education. In line with the standards, the course thematically draws from authentic texts surrounding Agricultural practices and food politics in East Africa. Topics to be covered have been selected carefully, in order to enable students acquire conversational, reading, and writing skills sufficient enough to engage in meaningful Swahili speech activities. The course will focus on comprehension and interpretation of Swahili oral and written texts and develop advanced grammatical and expository writing

Copyright UC Regents 2013

skills. Conversations and discussions will arise from the issues highlighted in the selected oral and written texts.

## MALENGO YA KOZI

### *Kuzungumza*

By the end of the semester a students should be able to:

- hold a conversation in a clearly participatory manner in order to communicate information on autobiographical topics, as well as topics of community, national, or international interest.
- handle topics concretely by means of narration and description in the major time frames of past, present, and future.
- deal with social situations with an unexpected complication.
- have abundant Swahili language output, her / his oral paragraph being the measure of length and discourse.
- have control of basic structures and generic vocabulary that they use should be understood by native speakers of the Swahili, including those unaccustomed to non-native speech.

### *Kuandika*

By the end of the semester a students should be able to:

- write routine informal and some formal correspondence, as well as narratives, descriptions, and summaries of a factual nature.
- narrate and describe in the major time frames of past, present, and future, using paraphrasing and elaboration to provide clarity.
- Students should be able to produce connected discourse of paragraph length and structure.
- show good control of the most frequently used structures and generic vocabulary, allowing them to be understood by those unaccustomed to the writing of non-native writers of Swahili.

### *Kusikiliza*

By the end of the semester a students should be able to:

- understand the main ideas and most supporting details in connected discourse on a variety of general interest topics, such as news stories, explanations, instructions, anecdotes, or travelogue descriptions.
- compensate for limitations in their lexical and structural control of the language by using real-world knowledge and contextual clues.
- derive some meaning from oral texts at higher levels if they possess significant familiarity with the topic or context.
- understand speech that is authentic and connected.
- demonstrate the ability to comprehend language on a range of topics of general interest.

- Portray sufficient knowledge of language structure to understand basic time-frame references.

***Reading***

By the end of the semester a student should be able to:

- understand the main idea and supporting details of authentic narrative and descriptive texts.
- compensate for limitations in their lexical and structural knowledge by using contextual clues.
- support their comprehension by knowledge of the conventions of Swahili language (e.g., noun/adjective agreement, verb placement, etc.).
- should be able to derive some meaning from straightforward argumentative texts (e.g., recognizing the main argument).
- Students should be able to understand texts that have a clear and predictable structure.
- demonstrate independence in their ability to read subject matter that is new to them since they will have sufficient control of standard linguistic conventions to understand sequencing, time frames and chronology.

At the beginning, the middle and the end of the course, you will be required to fill out evaluation forms about the course.

**MATINI ZINAZOHITAJIKA**

1. Awde, Nicholas. Swahili-English English-Swahili Dictionary, New York: Hippocrene Books,
2003.

2. Course packet to be provided by the instructor
4. Boner, E. Research on Agriculture and Food - conducted in Tanzania

**TATHMINI**

| | |
|---|---|
| 1. Class attendance, participation, homework and skit | 15% |
| 2. Short essays on issues encountered in the *texts* | 20 % |
| 3. Midterm exam | 15% |
| 4. Research project & presentation (Final exam 1) | 35% |
| 5. Term paper (based on your project) (Final exam 2) | 15% |
| **Total** | **100%** |

**ILANI**

Cheating of any kind is a serious university policy offence. You can work with others on assignments but be sure to always write your own answer(s). Be sure to express your concern about your performance (especially if you are having problems) early instead of late in the semester.

**WANAFUNZI WENYE ULEMAVU**
Students requesting classroom accommodation must first register with the Dean of Students Office. The Dean of Students Office will provide documentation to the student who must then provide this documentation to the instructor when requesting accommodation."

**ALAMA**
A+ 98-100: A 93-97: A- 90-92: B+ 87-89: B 83-86: B- 80-82: C+ 77-79: C 73-76: C- 70-72: D+ 67-69: D 63-66: D- 60-62: F 0-59

**MAHUDHURIO, KAZI YA NYUMBANI NA IGIZO LA TAMASHA 15%**
Attendance to all classes is essential. Since the objectives of the course are to develop advanced levels of communication, students must prepare well before class by reading and or listening the required texts in order to engage in meaningful discussion. In classes, a discussion of the text(s) will be done while at the same time addressing grammar issues that may arise from the texts. There will be an ongoing assessment of oral, listening, writing and reading proficiency skills in the classroom.

**INSHA FUPI 20%**
Every day, students will be expected to turn in (electronically), 100 word essays on issues raised from the texts. These essays must be typed, using font 12, and double-spaced. Essay

**MTIHANI WA KATIKATI YA MUHULA 15%**
For the midterm exam, the instructor will conduct an o**ral proficiency test**. The test will taking the form of a conversation between the instructor and test-taker. It will test how well a student speaks Swahili language by assessing her / his performance using ACTFL proficiency guidelines. During the test, the instructor will guide the conversation to explore the abilities and limits of a student's oral Swahili language abilities. During the course of the interview, the student taking Swahili will be guided to engage in a variety of tasks such as describing, narrating, and hypothesizing.

**KAZI YA UTAFITI NA KUWASILISHA 35%**
Students will be expected to choose a research topic of their choice on East African culture, social or political issues. Students are encouraged to use the media, specifically on-line newspapers, videos, film and music in their research. This project will be presented in class during the last two weeks. Students must consult the instructor once they have identified their topic. This project will be presented in Swahili language.

**INSHA YA MUHULA 15%**
Students will be required to write a term paper (a minimum of five pages) on a research topic of their choice on East African culture, social or political issues. This paper will be handed in during the exam week. More information will be given in class.

**RATIBA YA MASOMO**

| **WIKI** | **DARASANI** | **KAZI YA NYUMBANI** | **METHALI AU MSEMO WA WIKI** |
|---|---|---|---|
| WK 1<br><br>Th<br><br>08/29 | 1. Kujitambulisha<br>2. Kutoa maelezo ya silabasi<br>3. Kujaza hojaji ya kwanza | ***Utangulizi: Nyimbo za taifa za Afrika ya mashariki***<br>1. Andika insha ya maneno 100 kuhusu wimbo wa taifa wa Tanzania na Kenya<br>2. Sikiliza hotuba ya Rais Yoweri Museveni (dakika 5 za kwanza)<br><br>Wimbo wa taifa wa Tanzania<br>http://www.youtube.com/watch?v=MXpfDhgDKks<br>Wimbo wa taifa wa Kenya<br>http://www.youtube.com/watch?v=ovutwFN50TM<br>Workbook: Qn. 6 (p. 21), Qn.3, 4, (p.23-24) | Anayejitahidi hufaidi. |
| WK 2<br>Tue<br>09/03 | 1. Leta insha yako darasani<br>2. Wimbo wa taifa wa Kenya unahusu nini?<br>3. Wimbo wa taifa wa Tanzania unahusu nini?<br>4. Jitayarishe kuimba wimbo wa taifa darasani (kama unaweza)<br>5. Kujibu maswali ya wanafunzi kuhusu msamiati, sarufi, utamaduni kwenye nyimbo n.k<br>6. Sarufi:<br>a) Possessive<br>b) Proximant demonstarives | ***Kilimo katika Afrika ya Mashariki:***<br><br>Andika muhutasari wa maneno 100 kuhusu habari hii<br>http://www.voaswahili.com/content/bajeti-za-afrika-mashariki-zinawekeza-katika-kilimo-123489884/1362299.html<br><br>Workbook: Qn. 6 & 7 (p.24-25) | Akishindwa Sultani, raia huweza nini? |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | c) Subject prefixes<br>d) Relative prefix<br>e) Imperatives / Commands especially Kenya's national anthem.<br>f) The associative marker '-a' | | |
| Wed 09/04 | 1. Letainsha yako darasani.<br>2. Zungumza na rafiki yako kuhusu tofauti za uwekezaji katika kilimo nchini Marekani na katika nchi za Afrika ya mashariki<br>Sarufi:<br>(i) Prepositional (Applied) verbs<br>(ii) Passive voice | *Kilimo hai (organic) nchini Tanzania*<br><br>1. Sikiliza video ya kilimo hai<br>2. Andika insha ya maneno 100 kuhusu video yenyewe.<br>http://www.youtube.com/watch?v=CZuvYacJc84<br><br>Maswali:<br>(i) Kilimo hai ni nini?<br>(ii) Je kuna tofauti ya kilimo hali na kilimo cha kemikali?<br>(iii) Je, kilimo hai kina faida gani?<br>(iv) Kilimo cha kutumia kemikali kina faida yoyote?<br>(v) Je, ni nini maoni ya Janet Mara kuhusu kilimo hai?<br>(vi) Shirika lake Janet Mara linafanya kazi gani?<br>(vii) Ni magonjwa yapi yanayosababishwa kwa kutumia kemikali?<br>(viii) Ni kitu gani kinastahili kufanywa ili kuhamasisha Watanzania kuhusu umuhimu wa kilimo hai?<br>(ix) Watu wanaoishi Morogoro wameathirika vipi kutokana na wakulima milimani kutumia mbolea za kemikali?<br>(x) Inawezekana wakulima Tanzania kupoteza mazao yao wanapotumia mbolea za kemikali?<br>(xi) Mazingira yanaathirika vipi wakulima | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | wanapotumia mbolea za kemikali?<br>(xii) Serikali inaweza kuwasaidia vipi wakulima?<br>(xiii) Ni vyakula vipi vya bei rahisi: Ni vinavyotokana na kemikali au kilimo hai?<br>(xiv) Linganisha kilimo Tanzania na kilimo nchini Marekani.<br><br>Workbook: Qn. 1 & 3 (p. 27-28) | |
| Th 09/05 | 1.Leta insha yako darasani<br>2.Kuna tofauti gani za kilimo hai nchini Tanzania na kilimo hai nchini Marekani<br>3. Kujibu maswali ya wanafunzi kuhusu sarufi | *Umuhimu wa mbegu bora*<br>Andika muhutasari wa maneno 100 kuhusu habari hii<br>http://zanzibarkwetu.wordpress.com/2012/03/07/hutuba-ya-rais-ya-mkutano-wa-mbegu/<br><br>Workbook: Qn. 5 & 7 & 8(p. 28-30) | Atakaye kufuga n'gombe aanze na kuku |
| WK 3 Tue 09/10 | 1. Leta insha yako darasani.<br>2. Je, kuna umuhimu gani wa kuwa na mbegu bora?<br>3. Kuna tofauti gani ya mbegu zinazotumika nchini Tanzania na nchini Marekani<br>4. Kujibu maswali ya wanafunzi kuhusu sarufi | *Matatizo yanayowakumba waaandishi wa vitabu vya Kiswahili nchini Kenya (GOOGLE SEARCH)*<br><br>*Nordic Journal of African Studies 15(2): 143–153 (2006*<br><br>Soma uk. 145 – 150 (Matatizo) na uandike muhutasari wa maneno 100<br><br>Workbook: Qn. 1 (p. 31)<br>Maswali:<br>1. Waandishi chipukizi wa vitabu vya Kiswahili wanaathirika vipi na sekta ya uchapishaji?<br>2. Wizara ya elimu na saayansi pamoja na taasisi ya elimu ya KIE zinaathiri vipi uchapishaji?<br>3. Ukosefu wa soko la vitabu vya Kiswahili unaathiri vipi uchapishaji?<br>Baadhi ya maneno mapya:<br>Kilio, ufaafu, ikateuliwa, kushadidi, mtego, nyoyo, akiandika, kitaaluma, hujajulikana, | Wema hauozi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | uchapishaji, mswada, njaa ya vitabu, kujinyima, kitaaluma, mrabaha, kwa minajili, yategemewayo, pembeni, umeibua, tabia, kiwango, hoja,<br><br>Grammar notes: reflexive ji, 'ka' of order of things, ufaafu vs kilio ---abstract vs not abstract, ki-taaluma of manner, njaa ya vitabu ---expression, yategemewayo---2nd format of relative clause used with present tense only. | |
| Wed 09/11 | 1. Leta insha yako darasani.<br>2. Zungumza kuhusu matatizo yanayowakumba waandishi wa vitabu vya Kiswahili nchini Kenya.<br>3.Linganisha matatizo wa waandishi wa vitabu Marekani na waandishi wa vitabu nchini Kenya. Marekani<br>4. Kujibu maswali ya wanafunzi kuhusu sarufi | *Matatizo ya umeme katika nchi za Afrika ya Mashariki - Tanesco*<br>*http://www.youtube.com/watch?v=odPeCxNP3as*<br><br>**Transcript:**<br>Hayo yamebainishwa na kaimu meneja wa TANESCO kanda ya ziwa, Mhandisi Engineer Lucas Bunge wakati alipotembelea kituo cha umeme cha Nyakato jijini Mwanza na kujionea, hali halisi ya kazi zinazofanyika, usiku na mchana kwa lengo la kurejesha huduma ya nishati ya umeme kwa haraka katika mkoa wa Mwanza, Simiyu, Mala na Geita ambazo kwa sasa zipo gizani.<br>……<br>Kwa upande wake, mhandisi mkuu wa TANESCO mkoa wa Mwanza, Engineer Gerison Manase, amesema kuwa kutokana na hali hiyo ya mgao wa nishati ya umeme, TANESCO wamelazimika kuongeza mafundi, wakifanya kazi usiku na mchana kwa lengo la kurejesha huduma hiyo kwa wananchi kabla ya jumatatu.<br>…..<br>Nikiripoti kutoka Nyakato jijini Mwanza, Cosmas Makongo wa ITV<br><br>Maswali<br>1. Kituo cha umeme cha Nyakato kipo jiji gani<br>2. Kwanini kazi katika kituo cha umeme cha Nyakato inafanywa usiku na mchana?<br>3. Taja baadhi ya sehemuambazo hazina umeme? | Haraka haraka haina baraka |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 4. Andika insha ukilinganisha taabu za umeme nchi Marekani na katika nchi za Afrika ya Mashariki<br>5. Andika msamiati mpya na sarufi ambayo huifahamu<br>6. Sikiliza na ujaze sehemu zilizoachwa wazi<br>Hayo _______________ na kaimu meneja wa TANESCO kanda ya ziwa, ____________ Engineer Lucas Bunge wakati alipotembelea kituo cha __________cha Nyakato jijini Mwanza na kujionea, hali halisi ya kazi ______________, usiku na mchana kwa lengo la kurejesha huduma ya nishati ya umeme kwa haraka katika __________ wa Mwanza, Simiyu, Mala na Geita ambazo kwa sasa zipo gizani.<br>……<br>Kwa upande wake, mhandisi __________ wa TANESCO mkoa wa Mwanza, Engineer Gerison Manase, _________ kuwa kutokana na hali hiyo ya mgao wa nishati ya umeme, TANESCO wamelazimika __________ mafundi, wakifanya kazi usiku na mchana kwa lengo la ___________ huduma hiyo kwa wananchi kabla ya jumatatu.<br><br>Observations:<br>1.Student had issues with the adjectives '-ingi', and '-ingine', the associative marker '-a', possessive pronouns and adjective '-zuri' for all noun classes. Present negative.<br>2. Students had issues with colors in Swahili.<br><br>Msamiati mpya:<br>Hali halisi, kaimu meneja, huduma ya nishati ya umeme, mgao, gizani, kurejesha, kuongeza, nikiripoti.<br>Workbook: Qn. 3 (p. 32-33) | |
| **WK 4 M 09/16** | 1. Zungumza kuhusu ukosefu wa umeme nchini Tanzania na matatizo yake.<br>2. Kujibu | *Fasihi: Tamthilia ya KIBALI- David Kyeu* (utapokea nakala)<br>1. Soma kurasa tatu-saba za mwanzo za KIBALI<br><br>Maswali:<br>1. Tafsiri maneno yaliyoandikwa kwa herufi za | Akishindwa Sultani, raia huweza nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | maswali ya wanafunzi kuhusu sarufi<br>3. Kuandika insha kuhusu matatizo ya umeme nchini Marekani na Afrika ya mashariki | mlazo (italics)<br><br>*(Ni nyumbani kwa Bw. Ume. Chumba kimepambwa vizuri. Ukutani kunazo picha nyingi za Bi Kisasa akiwa chuoni akipokea zawadi mbalimbali. Ukuta wa upande wa nyuma kunazo picha za wanawe wawili: Karembo na Boi. Bi Kisasa ameketi upande wa kushoto. Anapekua vyeti vyake. Ume mumewe ameketi katika sofa iliyoko upande wa kulia.)*<br><br>2. Taja na ueleze baadhi ya msamiati usiofahamu kwenye kurasa 3 za mwanzo.<br><br>3. Taja baadhi ya maswala ya utamaduni wa watu wa kutoka Afrika ya mashariki ambayo yapo kwenye tamthilia. Je, maswala haya ya utamaduni yanatofautiana vipi na utamaduni wako?<br><br>4. Bwana Ume analalamika kwa nini? Taja baadhi ya malamiko.<br><br>5. Bi Kisasa anajitetea vipi kutokana na malalamiko ya mumewe Ume?<br><br>6. Je, kwa maoni yako unadhani Bw. Ume alimbaka mke wake Kisasa?<br><br>7. Katika uandishi wa tamthilia, majina ya wahusika mara nyingi hubeba sifa za wahusika. Je, ni kweli kuhusu majina ya Ume na Kisasa?<br><br>8. Andika sarufi mpya na msamiati mpya.<br><br>9. Andika insha ya maneno 70-100 kuhusu tofauti za utamaduni wa watu wa Afrika ya mashariki na wamarekani kwenye kurasa tatu ulizosoma.<br><br>Msamiati mpya na sarufi: Uliyoizoea (STROV), Ki-mapenzi(‘ki’ of manner), the ‘po’ of when, mkewe (contraction mke+wake), tangu (from when), dharau (contempt), uitakia-po (‘po’ of place), kinachokukaza, akijisemea (combination of ‘ki’ of when and the reflexive | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 'ji', pronouncing enhe!, asilani (the equivalent of hata kidogo, Abadan kataan), nifafanulie (subjunctive), uhusiano, sarakasi, ngono, anapekua, ku-to-kuwa (negating infinitives (monosyllabic) with 'to'<br><br>Workbook: Qn. 5 & 6 (p. 33-34)<br>Majibu ya sarufi ya leo<br><br><br>5. a) Kwa sababu gani hamsomi vitabu<br>b) Wanafunzi wana njia mbalimbali za kufanya mazoezi ya nyumbani<br>c) Wakulima wanakaa mbali na malori yao<br>d) Wao hawasafiri kwa ndege kwa sababu ni wagonjwa kidogo<br>e) Ingawa hawana pesa, wao wana elimu<br><br>6. a) The students are coming by bicycles to learn<br>b) By what means do you learn Swahili<br>c) S/he is studying because s/he is a good student<br>d) Why/For what reason is she coming today?<br>e) Speak in Arabic please<br>f) The city and the market are far from home | |
| **W 09/18** | 1.Zungumza kuhusu kurasa tatu za kwanza za tamthilia ya *Kibali*<br>*2.* Kujibu maswali ya wanafunzi kuhusu sarufi<br>3. Kuandika tamthilia fupi. | *Dini za Afrika ya Mashariki*<br><br>1.Soma Qur'an tukufu<br>[http://quranitukufu.net/001.html](http://quranitukufu.net/001.html)<br><br>2. Soma Biblia takatifu<br>[http://www.biblegateway.com/passage/?search=Tito+1&version=SNT](http://www.biblegateway.com/passage/?search=Tito+1&version=SNT)<br><br><br>Maswali:<br>1. Tafsiri sehemu hii kwa Kiingereza<br><br>*Sura hii iliteremka Makka kabla ya Hijra, kuhamia Mtume s.a.w. Madina. Imeitwa Al-Faatih'a, yaani Kifungulio kwa kuwa ndiyo sura ya mwanzo katika mpango wa Msahafu Mtukufu, nayo ni sura ya mwanzo iliyo teremka kwa utimilivu wake. Na sura hii inakusanya* | Atakaye kufuga n'gombe aanze na kuku |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | *jumla ya yaliyomo katika Qur'ani na kama kwamba huu ni mukhtasari wake, na baadaye yatakuja mambo kwa tafsili, babu-babu.*<br>*Na makusudio ya Qur'ani ni: Kubainisha Tawhid, Upweke wa Mwenyezi Mungu; na kubainisha ahadi na bishara kwa Muumini mtenda mema; na kubainisha ahadi na onyo kwa kafiri na mtenda maovu; na kubainisha ibada; na kubainisha njia ya kufanikiwa duniani na Akhera; na hadithi za walio mt'ii Mwenyezi Mungu wakafuzu, na hadithi za walio muasi wakaangamia.*<br>*Sura Al-Faatih'a inakusanya kwa ufupi na kwa kuashiria makusudio haya, na kwa hivyo ndio ikaitwa pia "Ummul Kitaab" yaani "Msingi wa Kitabu".*<br><br>(This chapter came down to Mecca, before the Hijra, the journey of the messenger (peace be upon him) to Medina. It was called Al-Faatih'a, i.e. the Opener, because it is the first chapter in the plan of Allah, and is the first chapter which came down in its completion. And this chapter gathers together the contents in the Qur'an and like that this is its summar, and later will come the things of interpretation. And the objectives of the Qur'an are: to explain Tawhid, the oneness of Allah; and to explain the promise and benefits for the Believer and good doer; and to explain the promise and warning for the infidel and evil doer; and to explain religious service; and to explain the way of succeeding in the world and the afterlife; and stories of followers of Allah who then succeeded, and stories of dis-believers who then got destroyed.)<br>(Translated byDavid Kyeu and Caroline Ritter UC Berkeley)<br><br>2. Zungumza kwa ujumla (toa maoni yako) kuhusu surah ii ya Quran.<br><br>3. Nini maoni yako kuhusu mstari huu kutoka kwenye biblia: "15 Kwa watu waliosafi kila kitu ni safi. Lakini kwa watu waovu na wasioamini hakuna kilicho safi." | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 4. Nini maoni yako kuhusu mstari huu kutoka kwenye sura Al-fatha (Quran)<br>“Kubainisha ahadi na bishara kwa muumini mtenda mema; na kubainisha ahadi na onyo kwa kafiri na mtenda maovu.”<br><br>4. Taja na ueleze baadhi ya msamiati na sarufi mpya kwenye sura hii ya al-fatha.<br><br>5. Taja na ueleze baadhi ya msamiati na sarufi mpya kwenye Biblia (Tito 1)<br><br>6. Andika insha ya maneno 100, ukilinganisha maandishi ya Quran na maandishi ya Biblia uliyosoma.<br><br>**Msamiati na sarufi mpya kutoka kwenye Tito 1 (Biblia):**<br>Ninakutakia neema- I wish you grace<br>Naye- Contraction of Na and Yeye<br>Mwanangu – Contraction of Mwana and Wangu<br>uzima wa milele- eternal life<br>Urekebishe- you rectfy/you correct,<br>hayakunyooka-they were not straight,<br>nilivyokuagiza- they way I instructed you,<br>jeuri na wasiotii-Sturborn and disrepsectiful ,<br>umekabidhiwa-You have been given,<br>anapaswa-S/he is supposed,<br>mwepesi wa hasira-Easily angered,<br>kujitawala-to rule yourself,<br>kudhibiti nafsi yake-To control him/herself,<br>uthabiti-Strength,<br>kikundi cha tohara-the circumcision group,<br>wasiyostahili kufundisha-Those they don’t need to teach,<br>wajipatie fedha-they get money for themselves<br>uwakemee kwa ukali-rebuke them strongly,<br>wasiendelee kushikila hadithi za kiyahudi-they should not continue holding on jewish stories,<br>dhamiri-lengo,nia (intention/objective)<br><br>**Msamiati na sarufi mpya kutoka kwenye Sura Al-fatha (Qur’ani)** | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Iliteremka- it came down / it descended<br>Makka-Mecca,<br>Hijra- is the migration or journey of the Islamic prophet Muhammad and his followers from Mecca to Medina between June 21 and July 2 in 622 AD.<br>Kuhamia-change position to / relocate<br>Mtume S.A.W. – The messenger, in accordance with the Arabic words *sallallahu alayhi wasallam---peace be upon him*<br>Madina – Madina (Gegraphical space in the middle east<br>Msahafu mtukufu-Holy book (religious),<br>utimilifu wake- in its entirety,<br>tafsili babu-babu-explicit translation,<br>kubainisha-to explain,<br>Tawhid—the oneness of God, in the sense that he is one and there is no god but he<br>Bishara-faida (benefit)<br>Akhera-Islamic term referring to the after life<br>waliomtii mwenyezi Mungu-those who respected the almighty God<br>wa-ka-fuzu-they graduated (-ka- tense of verb sequence<br>wa-ka-angamia-they got destroyed-'ka' tense of verb sequence<br>mwingi wa rehema-full of mercy<br>mwenye kurehemu-the one who is merciful,<br>mlezi-Guardian<br>viumbe vyote (Viumbe wote grammatically correct – all creation<br>kumiliki-to own<br>siku ya malipo-the day of payment/the day of judgement<br>tunakuabudu-we worship you<br>tuongoe –lead us<br>iliyonyooka-the one which is straight<br><br>**Proverb of the week:**<br><br>Atakaye kufuga n'gombe aanze na kuku kwanza<br>Anyone who wants to rear a cow, should first start with chicken | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Workbook: Workbook: Qn. 4 & 5 (p. 36)<br>4. Andika kwa kukataa (Negate)<br>a) Sitaanza kufunza saa nne<br>b) Hatutasoma Kiswahili kesho<br>c)Hutafanaya kazi mwezi wan ne<br>d)Hamtafahamu Kiingereza vizuri<br>e)Hatakula chakula chake chote<br>f)Hawataenda kufanya utafiti Kenya<br><br>5. Andika kwa wingi (Plural)<br>a) Wao hawawezi kwenda kwa baiskeli<br>b)Je, hatutaweza kuondoka saa mbili?<br>c) Madereva hawataondoka upesi sana.<br>d) Kwa hivyo hamtaamka saa kumi na moja alfajiri.<br>e) Baba zao watakwenda kuvua samaki<br>f) Sisi hatutaanza kusoma katika vyuo vikuu<br>g) Je, mtasimama mara kwa mara katika vituo mbalimbali. | |
| **WK 5<br>M<br>09/23** | 1. Leta insha yako darasani.<br>2. Je, habari kutoka kwenye Qur'an tukufu, yanahusu nini?<br>3.<br>6. Kujibu maswali ya wanafunzi kuhusu sarufi | *Ugaidi katika Afrika ya Mashariki: Shambulizi Westgate Mall mjini Nairobi*<br>*http://www.youtube.com/watch?v=nNyQ89GiSoA*<br><br>Hivi ndivyo hali ilivyokuwa katika jengo la Westgate, watu wengi walikuwa wamefika kwa Shughuli mbalimbali. Ikiwa ni pamoja na ununuzi wa bidhaa na kujipumzisha mikahawani. Na mara wakakatizwa. Judith Otunga na Charles Mwova ni baadhi ya walioshudia matukio ya awali katika duka hili mwendo wa saa saba. "Nilikuja nikadrop boss yangu opposite ya main gate ya hiyo shida penye imetokea. After my boss kuingia ndani nilisikia mlio wa risasi. By kwa hivyo wakati mimi nilifungua mlango na nikaingia chini ya gari." Wanadai wavamizi walikuwa wanaume karibu kumi waliovalia kanzu huku wakiwa wamefunika nyuso zao. "Kuna gari zilikuwa tatu. Gari moja ilikuwa Probox ya white, ilikuja ikafunguliwa milango yote by hapo ndipo nikaanza kusikia marisasi na sasa ikawa kila mtu yote ni kujisaidia vile mtu anaweza." Judithi Otunga alikuwa ametoka katika duka moja humo ndani na anasema alinusurika tu. | Wema hauozi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | “Sasa niilikuwa nakuja hivi nikapitia Café ati kununua mkate, nikafika kwa stairs, kuteremka hivi kidogo nikaanza kuona watu wakikimbia, Nikashangaa hawa watu wa Westgate wanapenda kushtua watu na mbio. Sijui nini kinaendelea. Within two minutes nikasikia kitu kama imelipu…imelipuka.” Huku idadi kamili ya walitekeleza maovu hayo bado haijatambulika. Kilicho bayana ni huku wengine wakianza mashambulizi nje, wengine walikuwa ndani. “ Walianzia kwa maingate, hapo ndipo walianza kuninii…entrance ya kuingia ndio walianza kuchut…kushoot hapo na vyenye walikuja walikuja na spidi nyingi hata hawakuwa wanapatia mtu ruhusa ya kuongea.” Takriban masaa sita baadaye bado walionusurika wanazidi kutolewa katika jengo hili wakiwa wameshuhudia ambayo wengi hawawezi kuyaeleza. Waliokuwa wameumia walikimbizwa mahospitali, walionusurika bila majeraha wakazuiliwa kwa muda na kuhojiwa. Kulikuwepo na walinda usalama kutoka kila kitengo hata wanajeshi. Wote wakijaribu kuthibiti hali hiyo. Charles anasema mwajiri wake yuko salama. “Ameponea, saa hii ako safe na amenipigia simu akasema sawa kama tuko hai Mungu ni mzuri. Nia ya wavamizi bado haijulikani wengi hata hivyo wanasema ni kitendo cha kigaidi. Andrew Ochieng. NTV<br><br>*Maswali*<br>1. Sikiliza na ujaze sehemu zilizoachwa wazi.<br><br>Hivi _________ hali ilivyokuwa katika _______ la Westgate, watu wengi __________ wamefika kwa<br>Shughuli mbalimbali. Ikiwa ni pamoja na _________ wa bidhaa na kujipumzisha mikahawani. Na mara _________. Judith Otunga na Charles Mwova ni baadhi ya _________ matukio ya awali katika duka hili mwendo wa saa __________.<br><br>2. Sikiliza na ujaze sehemu zilizoachwa wazi<br>. “ Walianzia _______ maingate, hapo ndipo __________ kuninii…entrance ya kuingia ndio | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | _________ kuchut…kushoot hapo na vyenye walikuja walikuja na spidi ________hata hawakuwa wanapatia mtu _________ ya kuongea.”<br><br>3. Sikiliza na ujaze sehemu zilizoachwa wazi __________ masaa sita baadaye bado walionusurika wanazidi ___________ katika jengo hili wakiwa wameshuhudia ambayo wengi ____________kuyaeleza. Waliokuwa wameumia walikimbizwa mahospitali, walionusurika bila majeraha ____________ kwa muda na kuhojiwa. Kulikuwepo na walinda usalama ___________ kila kitengo hata wanajeshi. Wote wakijaribu kuthibiti hali hiyo. Charles anasema __________ wake yuko salama.<br><br>4. Tafsiri sentensi hii kutoka kwenye habari “Wanadai wavamizi walikuwa wanaume karibu kumi waliovalia kanzu huku wakiwa wamefunika nyuso zao.”<br>______________________________________<br>______________________________________<br>______________________________________<br>______________________________________<br><br>5. Zungumza kuhusu tukio hili la ugaidi na ulinganishe na matukio ya ugaidi katika nchi yako<br>6. Andika insha ya maneno 100 kuhusu ugaidi katika Afrika ya mashariki na katika nchi ya Marekani<br>7. Taja na ueleze baadhi ya msamiati na sarufi mpya kwenye habari<br><br>Msamiati na sarufi mpya<br>Shughuli mbalimbali – various activities<br>Walioshuhudia- those who witnessed<br>Matukio – events<br>Mlio wa risasi – bullet sound<br>Wanadai – They claim<br>Wavamizi – attackers<br>Kanzu – Robe<br>Marisasi – Bullets<br>Alinusurika – S/he escaped unhurt | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Idadi kamili- the correct number<br>Mashambulizi – attacks<br>Spidi – speed<br>Ruhusa – chance<br>Takriban – Almost<br>Walionusurika wanazidi kutolewa – those who escaped unhurt are continuing to be removed<br>Kuhojiwa- to be interviewed<br>Haijulikani – its not known<br><br><br>Workbook: Qn. 6 & 7 (p. 36-37) | |
| **W 09/25** | | | |
| **WK 6 M 09/30** | 1. Zungumza kuhusu uchapishaji wa habari nchini Tanzania. mashariki na Marekani.<br>2. Kujibu maswali ya wanafunzi kuhusu sarufi<br>3. Andika insha kuhusu uchapishaji nchini Marekani na katika nchi za Afrika ya mashariki | *Haki za binadamu katika Afrika ya mashariki*<br><br>*1. Ushoga nchini Kenya na nchini Tanzania*<br><br>*http://www.youtube.com/watch?v=kPrVAWHlG8w*<br><br>*Maombi yako kwa serikali ni nini? Maombi yangu ni kuwa pia sisi watufikirie. Eeeh watufikirie, kila mtu na maisha yake. Kila mtu na maisha yake na jinsi anajipatia riziki yake. Sasa wasitutenge, wasitulaumu na wasitudhulumu. Tupewe haki zetu na pia sisi tuone raha…..Kwa raha zetu, ushoga ndio huo. Twasikia uchungu sana, tunanyanyaswa. Twasikia uchungu. Ni vile sisi ni crony. Hatutaki kujua waziri atasema nini. Kama atakubali, hakubali ni maisha yetu. Tumechoka, ni maisha yetu haya. Tumeamua tujiuze mpaka dakika ya mwisho.*<br><br>*1. Tafsiri kifungu hiki kwa Kiingereza*<br><br>*2. Je, kuna msamiati na sarufi ambayo ni gumu kuelewa?*<br><br>*http://www.youtube.com/watch?v=vmZfJUYcHmk*<br><br>*1. Je, habari zinatangazwa na shirika lipi la utangazaji?* | Haraka haraka haina baraka |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | *2. Tanzania imesema haiko tayari kufanya nini?*<br><br>*3. Waziri mkuu wa Uingereza, Bwana David, Cameroon alitoa tamko gani?*<br><br>*4. Mheshimiwa Bernard Mende ni nani?*<br><br>*5. Mheshimiwa Mende amesema utoaji misaada unaunganishwa na nini?*<br><br>*6. Mheshimiwa Mende amesema nchi ya Tanzania inafuata utamaduni gani?*<br><br>*7. dakika 2.52 – 3.45*<br>*Nadhani ni muhimu kabisa kwa Watanzania wakati huu ambapo tunajiandaa kuandika katiba mpya kufikiria kwa kina ni kwa namna gani tunaweza kuweka kwenye katiba yetu vipengele ambavyo vitatupa mwongozo kwa jinsi ambapo Tanzania itakuwa na mashirikiano na misimamo yake na nchi nyingine lakini zaidi ikaelekeza linapokuja swala la misaada ya aina gani Watanzania wapokee kwa sababu jambo hili kwa nchi kama ya kwetu, ambayo ni nchi tajiri kiasi hiki si nchi ya kunyanyaswa kwa ajili ya misaada.*<br><br>*Sikiliza na ujaze sehemu zilizoachwa wazi*<br><br>*dakika 2.52 – 3.45*<br>*Nadhani ni __________ kabisa kwa Watanzania wakati huu ambapo tunajiandaa kuandika ____________ mpya kufikiria kwa kina ni kwa namna gani tunaweza kuweka kwenye katiba yetu ___________ ambavyo vitatupa mwongozo kwa jinsi ambapo Tanzania itakuwa na mashirikiano na misimamo yake na nchi ___________ lakini zaidi ikaelekeza linapokuja swala la misaada ya aina gani Watanzania wapokee kwa sababu jambo hili kwa ________ kama ya kwetu, ambayo ni nchi tajiri kiasi hiki si nchi ya _______________ kwa ajili ya misaada.* | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | *8. Zungumza na mwenzako ukilinganisha ushoga katika nchi za Afrika ya mashariki na nchi yako*<br><br>*9.Baada ya kuzungumza andika insha ya maneno 100 ukilinganisha ushoga katika Afrika ya mashariki nan chi yako.*<br><br>**Sarufi kutoka kwenye video**<br><br><u>Subjunctive:</u><br>(a) Used after verbs of 'telling', 'ordering' and 'wanting'. It is used in the context where the subject of the main verb (of telling, wanting, etc.) and the subordinate verb are different. (Hinnebusch & Mirza: 149)<br><br>Examples<br>**(i)** Ataniambia nipik**e**<br>(ii) Anawataka mlal**e**<br><br>**(b)** After *afadhali* 'it would better'<br>Examples<br>**(i)** (Ni) afadhali nisome.<br>**(ii)** (Ni) afadhali watoto wacheze.<br><br>(c) After *ili* 'inorder that'<br><br>Example<br>(i) Anafanya hivi **ili** niondoke hapa.<br><br>(d) When the subject of the first verb is distinct *clauses*from the subject of the second verb. Contrast the two sentences below:<br><br>(i) Ninataka kupika 'I want to cook'<br>(ii) Nina(wa)taka wapike. 'I want them to cook'<br><br>(e) To ask permission, to express obligation and to make requests: p. 170<br><br>Examples<br>(i) Nitafsiri kitabu hiki? 'May I translate this book?'<br>(ii) Tule chakula gani? 'What food do wee | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | need to eat?’<br>(iii) Tupike sasa? ‘Should we cook now?’<br><br>(f) Used after mpaka ‘until, upto, as far as’ to express *results clauses in English that are introduced by the conjuction ‘until’*<br><br>**Msamiati mpya kutoka kwenye video**<br>Watufikirie-They should think about us<br>Jinsi-how/the way/manner<br>Anajipatia-S/he gets for herself / himself<br>Riziki-fortune<br>Wasitutenge- They should not segregate us<br>Wasitulaumu- The should not blame us<br>Wasitudhulumu – They should not bother us<br>Tupewe<br><br><br><br>*Workbook: Qn. 8 (p. 37-38)* | |
| **Wed 10/02** | | *Quiz # 1*<br><br>*i. Sarufi (Grammar)*<br><br>*1. Tafsiri kifungu hiki kwa kiingereza (Alama 10)*<br><br>*Sura hii iliteremka Makka kabla ya Hijra, kuhamia Mtume s.a.w. Madina. Imeitwa Al-Faatih'a, yaani Kifungulio kwa kuwa ndiyo sura ya mwanzo katika mpango wa Msahafu Mtukufu, nayo ni sura ya mwanzo iliyo teremka kwa utimilivu wake. Na sura hii inakusanya jumla ya yaliyomo katika Qur'ani na kama kwamba huu ni mukhtasari wake, na baadaye yatakuja mambo kwa tafsili, babu-babu.*<br>*Na makusudio ya Qur'ani ni: Kubainisha Tawhid, Upweke wa Mwenyezi Mungu; na kubainisha ahadi na bishara kwa Muumini mtenda mema; na kubainisha ahadi na onyo kwa kafiri na mtenda maovu; na kubainisha ibada; na kubainisha njia ya kufanikiwa duniani na Akhera; na hadithi za walio mt'ii Mwenyezi Mungu wakafuzu, na hadithi za walio muasi wakaangamia.* | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | *2. Andika kwa kukataa (Negate) (Alama 6)*<br>*a) Nitaanza kufunza saa nne*<br>*b) Tututasoma Kiswahili kesho*<br>*c)Utafanaya kazi mwezi wan ne*<br>*d)Mtafahamu Kiingereza vizuri*<br>*e)Tutakula chakula chake chote*<br>*f)Waataenda kufanya utafiti Kenya*<br><br>*ii. Kuzungumza kwa dakika 10 (10 minutes interactive conversation) (Alama 10)*<br><br>*Wewe na rafiki yako zungumza kuhusu matukio ya ugaidi katika nchi za Afrika ya mashariki na ulinganishe na matukio ya ugaidi katika nchi yako*<br><br>*iii. Kusikiliza (Listening )*<br><br>*1. Sikiliza na ujaze sehemu zilizoachwa wazi (Alama 5)*<br><br>*http://www.youtube.com/watch?v=odPeCxNP3as*<br><br>*Hayo ________________ na kaimu meneja wa TANESCO kanda ya ziwa, _____________ Engineer Lucas Bunge wakati alipotembelea kituo cha ___________cha Nyakato jijini Mwanza na kujionea, hali halisi ya kazi _______________, usiku na mchana kwa lengo la kurejesha huduma ya nishati ya umeme kwa haraka katika ___________ wa Mwanza, Simiyu, Mala na Geita ambazo kwa sasa zipo gizani.*<br><br>*iv. Kuandika insha ya maneno 250-300 (essay writing of 300 words) (Alama 20)*<br><br>*Andika insha ya maneno200- 300 kuhusu mada ya matukio ya ugaidi uliyozungumza na rafiki yako* | |

| | | | |
|---|---|---|---|
